

# Yesu Ni Mtulivu!

THIS IS A MESSAGE OF LOVE, AND WITH LOVE

IT IS BROUGHT TO YOU BY


SAJU

JOHN MATHEW

Visit: www.sjmathew.com



A PRODUCT OF:

SANCTUARY

Word Media Publishing Pvt. Ltd.

# Yesu Ni Mtulivu!



Mpendwa Billy, Ninataka kuwa Mkristo. Lakini kabla ya hapo, Ninataka vitu vya kunifurahisha…" Kitabu kiitwacho "Ndugu Billy" (Maswali kwa Billy Graham) huanza na swali hili, ambalo liliulizwa na binti mmoja. Je alimaanisha nini? Je haiwezekani Mkristo kuwa na vitu vya kufurahisha au kuchekesha katika maisha?

Inaweza ikaonekana kana kwamba iko hivyo, na hasa kama tukitazama nyuso za Wakristo wengi… "Ni watu wenye nyuso zisizo na tabasamu zenye kumaanisha" (Serious. Nakumbuka maombolezo ya  Osho katika moja ya hotuba zake ("Hakuna mzaha") na

kwamba nyuso zote za watu wa dini ni ndefu – hazionyeshi mzaha.

Angalia picha na hata sura za waanzilishi wa dini mbalimbali. Hazina nyuso zenye tabasamu! Mfano Buddha, Mahavira na Miungu yote ya dini za Mashariki zina nyuso ngumu kama wafuasi wao walivyo. Hawatabasamu, hawali, wala hawaimbi…

Lakini unafikiri nini juu ya Yesu? Ninahakika kwamba Yesu alikuwa wa tofauti nyakati alipoishi katika ulimwengu huu. Alikuwa tofauti kabisa na viongozi wa dini wa wakati wake. Alikuwa mtu wa "Kawaida" Aliishi kama watu wa kawaida; Alilala kama watu wa kawaida na alikuwa kama watu wa kawaida!

## Ucheshi ni Ubinadam

Yesu aliongea mambo makubwa, makubwa… Lakini katika njia ya utulivu sana. Soma Mathayo sura 13 utaona jinsi alivyofundisha kweli kubwa kuhusu ufalme wa Mungu katika njia rahisi sana. Misingi ya mifano yake ilijaa ucheshi. Je ungeweza kujizuia kufurahi unaposikia ngamia kupita tundu la sindano? Usingeweza kufurahi unaposikia habari za mtu aliyeanza mradi mkubwa wa ujenzi wa

mnara akiwa na pesa kidogo na akashindwa hata kuumaliza msingi?

Wakati Mwingine Alifunga, Wakati Mwingine Alisherehekea.



Yesu alisisitiza kuwa wanafunzi wake wafunge na kuomba, Lakini hakuwa kinyume na kushiriki sherehe wakati mwingine. Hata yeye alipenda sherehe. Nyingi ya mifano yake ilihusu sherehe. (Mathayo 22:2; Luka 13:21; 14:15). Mfano wake mashuhuri kuhusu “Mwanampotevu” unafikia kilele kwenye sherehe. Alikaribishwa kwenye sherehe mara nyingi na hakukataa. (Luka 7:36. “Mtu mmoja katika Mafarisayo alimwalika ale chakula



kwake; akaingia katika nyumba yake yule Farisayo, akaketi chakulani".

Lakini kumbuka, Yesu hakula peke yake. Huo ni ulafi. Karamu zilikuwa sehemu ya jamii na aliweza hata kuhudhuria baadhi ya arusi. Yesu hakuwa mlafi japo wengi walimwita hivyo.

## Rafiki wa Watoza Ushuru

Watu wa dini wa wakati wa Yesu hawakuwa tayari kuzungumza na wanawake mbele za watu. Wakati mwingine Mafarisayo walifunika macho yao kwa kitambaa walipokuwa wakitembea mitaani ili kwamba macho yao yasije kutazama wanawake. Kwa kawaida walijipigiza wenyewe juu ya kuta na vitu vingine vigumu pembeni mwa barabara na mara nyingi walitokwa na damu ("Waliitwa Mafarisayo watokwa damu"). Walichukulia hili kuwa ni ishara ya utakatifu (yaani huko kujitesa).


Lakini Yesu alijua yeye alikuwa nani? Hakufanya jambo lolote ili kuwapendeza wanadamu. Alimpenda kila mtu. Alizungumza na wanawake, hata na watu wenye hadhi ya chini. Kumbuka, Alitumia muda kuzungumza na mwanamke Msamaria hata wanafunzi wake wakashangazwa na hilo.



(Yohana 4:27: “Mara hiyo wakaja wanafunzi wake, wakastaajabu kwa sababu alikuwa akisema na Mwanamke; Lakini hakuna aliyesema unatafuta nini au “Mbona unasema naye?” Walijua, hata wakati Yesu alipokuwa mtu rahisi na wa kuingilika, alibakia kuwa Mtakatifu na bila mawaa.

Yesu alikuwa safi wa moyo na nafsi.
Hakuhitaji kushuhudiwa na wanafiki wa wakati wake.

Si kile watu wanasema kuhusu wewe kinachojalisha bali wewe halisi ulivyo ndilo la muhimu. Yesu aliwaambia wale wanafiki: “Kwa kuwa Yohana Mbatizaji alikuja hali mkate wala hanywi divai, nanyi mwasema,



`Ana pepo.' Mwana wa Adamu amekuja anakula na kunywa, nanyi mwasema, `Tazama mlafi huyu na mnywaji wa divai, rafiki wao Watoza Ushuru na wenye "dhambi". (Luka 7:33-34)"- Wenye dhambi hapa inamaanisha makahaba. Lilikuwa ni Neno la Kiaram. Tazama Neno linalofanana nalo, Mathayo 21:31: Yesu akawaambia, "Amini nawaambia, Watoza ushuru na Makahaba wanatangulia mbele yenu kuingia katika Ufalme wa Mungu". Kumbuka, Yesu aliishi maisha safi katika ulimwengu usio Mtakatifu. Aliwapenda wenye dhambi, lakini hakupenda dhambi!

## Uwe Mtulivu

Yesu alikuwa mtu kama sisi. Alikuwa na kujisikia kama wewe na mimi. Wakati mwingine alikuwa na furaha na mara kadha alihuzunika. Aliwahurumia watu waliokuwa kwenye matatizo. Hakujaribu kujifanya ana nguvu kwa kuzuia hisia zake. Alikuwa mtu wa kawaida aliyeonyesha hisia zake wazi wazi.

Yesu pia hakuweza kuchelewa kuonyesha furaha ya moyo wake. Wakati wanafunzi wake waliporudi kwa Mafanikio makubwa toka kwenye huduma hakujizuia roho yake kufurahi. ("Saa ile ile alishangilia kwa Roho Mtakatifu, akasema, "Nakushukuru Baba, Bwana wa Mbingu na Nchi". Luka 10:21)

Wakati rafiki yake Lazaro amekufa na dada zake walipokuwa wamefadhaika, Yesu alilia. kama binadamu! ("Basi Yesu alipomwona analia, na wale Wayahudi walifuatana naye wanalia, aliugua rohoni, akafadhaika roho yake...Yesu akalia machozi. Basi Wayahudi wakasema, angalia jinsi alivyompenda". (Yoh. 11:33-36)

## Rafiki wa Kila Mtu



Yesu aliweza kuhusiana na watu wa aina zote za maisha (Ngazi zote). Alikuwa rafiki wa kila mtu hata watoto. Baadhi ya watu walileta watoto kwa Yesu ili awaguse, lakini wanafunzi wake

wakawazuia. Yesu alipoliona hili alichukizwa sana akawambia wanafunzi wake, “Waacheni watoto wadogo waje kwangu msiwazuie, kwa maana Ufalme wa Mbinguni ni wao”. (Marko 10:13-14)

## Alipenda kuimba



Wengi hawaelewi kuwa Yesu alipenda kuimba. Alipenda Zaburi na mara nyingi alinukuu toka Zaburi. (zaburi zilikuwa ni Nyimbo za Wayahudi). Hata wakati wake wa mateso aliimba na wanafunzi wake.

(“Nao walipokwisha kuimba, wakatoka nje kwenda mlima wa mizeituni”. (Mathayo 26:30).

## Njoo, Petro, Tembea Juu ya Maji

Petro alipomwona Yesu akitembea juu ya maji, alitaka naye kufanya hivyo. Yesu hakumzuia! Hakusema uwezo huu maalum ni kwa ajili yangu tu. Alimruhusu Petro kutembea juu ya maji… Hakuwa na faida yoyote katika kufanya hivyo. Ilikuwa ni kwa ajili ya furaha tu… Lakini Yesu aliruhusu jambo hili.

Yesu alikuwa mtulivu. ("Hata wakati wa zamu ya nne ya usiku, Yesu akawaendea, akienda kwa miguu juu ya maji… "Petro akajibu akamwambia Bwana ikiwa ni wewe, "niamuru nije kwako juu ya maji." Akasema njoo! Petro akashuka chomboni akaenda kwa miguu juu ya maji ili kumwendea Yesu. (Mathayo 14:25-30)

Huyu Yesu anataka kuwa rafiki yako (Yohana 15:15) Kwa nini usifanye urafiki na Yesu? Yeye ni mtu mtulivu lakini anaita kwa karibu yenye uchangamfu.




**<u>Oh! Hapana! Mimi ni mwenye dhambi... Nawezaje Kuwa na Urafiki na Yesu? Hata kama aliishi kama mwanadamu katika ulimwengu huu, Yeye ni Mungu Mtakatifu!</u>**

Hivyo ndivyo unavyosema? Ni kweli kwa sehemu uko sawa… Yesu aliishi katika ulimwengu huu kama binadamu mfano wa wewe na mimi.  Lakini ni Mungu wa Milele! Ni kweli, Mtu mwenye dhambi hawezi kuwa na uhusiano na Mungu… Hata hivyo, Yesu alikuwa na mpango maalum wa kukuweka huru mbali na dhambi zako na kukufanya wewe uweze kuingia katika uhusiano na Mungu… Mpango wake ni kitu cha Ki-Mungu.



Aliamua kuchukua adhabu ya dhambi yako (Kama kwamba mtu fulani amelipa deni lako lote). Ndiyo maana Yesu alikuja katika ulimwengu huu... na kufa msalabani badala yako.Akabeba matokeo yote ya



dhambi na kukuweka huru mbali na hukumu. Yeye alifanya yote. Unachotakiwa kufanya wewe ni kumpokea. Kama mtu akikupa hundi, unatakiwa kuipokea na kuikubali, kwa kuweka saini ili iweze kulipwa. Kadhalika Yesu alikufa msalabani ili kukuweka wewe huru mbali na dhambi zako, hatia na mauti. Hata hivyo unatakiwa kukubali na kumkiri kwa kinywa chako…

Yule mtoza ushuru aliomba maombi mafupi. Alisimama mbali, hakuweza hata kuinua uso wake kuelekea Mbinguni, Lakini alipigapiga kifua chake na kusema, 'Mungu, Unirehemu mimi mwenye dhambi!' (Luka 18:13) na alisamehewa. Yule mwizi msalabani alimwomba tu Yesu amkumbuke, na mara Yesu akamwahidi kuwa pamoja na yeye peponi. (Luka 23:42-43) Petro alitubu kwa machozi kwamba alikuwa mwenye dhambi. Alifikia hata akasema Bwana, ondoka kwangu maana mimi ni mtu mwenye dhambi; Sistahili hata kukukaribia (Luka 5:8). Aliogopa kwamba Yesu angeweza kumwadhibu; kwa ajii ya dhambi zake. Hata hivyo Yesu

hakumsukumia mbali Petro, “Usiogope Petro, Yesu akasema; Nitakwenda kufanya urafiki na wewe. Nitakwenda kukufanya ulete watu kwa Mungu!” (Luka 5: 8-10)

**Oh! Hii ni ajabu! Unasema, Kama Nikimwomba Yesu atakuwa rafiki yangu sasa hivi? Je naweza kuokolewa toka dhambi zangu zote za zamani na kuishi maisha Matakatifu?**

Bila shaka rafiki yangu. Yesu ni mtu mtulivu. Yuko tayari kukubali na kukufanya kuwa rafiki yake Ulimwengu mpya kabisa unakusubiri. Ulimwengu wenye furaha, uhuru, utakatifu na Urafiki na Yesu. Kwa nini basi usizitubu dhambi zako na kumwomba yeye msamaha? Yesu atakufanya wewe kuwa rafiki yake, sasa hivi.

Hebu sema maneno haya:

***Yesu, mimi ni mwenye dhambi, nilikuwa nangojea hukumu…nilikuwa nimenaswa na hofu, hatia na aibu. Sasa, Ninafahamu kwamba, wewe unanipenda, mimi maskini, na uko tayari kunisamehe dhambi zangu na kunifanya rafiki yako. Najua sistahili jambo hili. Kitu pekee ninachoweza kuomba ni rehema zako***

***Bwana Yesu, unirehemu. Nifanye kuwa rafiki yako…Mimi ni wako, Amen!***

**Wako, Katika Jina la Yesu,**

**SAJU JOHN MATHEW**

**Tembelea: www.sjmathew.com**

Imetafsiriwa katika kiswahili na
**Mchungaji Moses Magembe**

Gospel Campaign Center
TAG MajumbaSita
P. O. Box 77313
Dar es Salaam, Tanzania, East Afrika

**Kama una maswali yoyote usisite kuwasiliana nasi:**

Simu:
Pastor Moses Magembe- +255 715 283819 / 784 283818
Capt. Siyame Paul- +255 767 359993
Barua pepe: gospeldsm@gmail.com

**Gospel Campaign Center**
**TAG MajumbaSita, P. O. Box 77313**
**Dar es Salaam, Tanzania, East Afrika**

